

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

SHULE YA SEKONDARI MISUFINI
S.L.P 73,
NACHINGWEA.

KUMB Na, MISS/HM/VOL.2/01

18/12/2020.

MZAZI/MLEZI WA

.....

YAH. KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA 1 MWAKA 2021.

UTANGULIZI:

Kwa niaba ya uongozi na wafanyakazi wote wa Misufini sekondari nachukua fursa hii kumpongeza mwanao kwa kuchaguliwa kujiunga na sekondari ya MISUFINI.

Misufini sekondari ipo katikati ya kijiji cha mkumba na Mpiruka kilometa 3, kaskazini masharikki mwa kituo cha utafiti wa kilimo cha Mkumba.

Kijana wako amechaguliwa kujiunga na shule hii.Matarajio yetu HATAIPOSEZA NAFASI HII NYETI KWAKE,Pia wewe mzazi/mlezi niwajibu wako kumwandaa kijana wako ili aweze kumudu changamoto za shule na kuhakikisha anaendelea hadi kidato cha nne.

Ndugu mzazi/mlezi KAMWE husimkoseshe mtoto haki ya kupata ELIMU kwa kisingizio cha UMASIKINI au kipato DUNI,aidha ni wajibu wako kumuasa kijana wako kuwa ELIMU ndio ufunguo wa maisha.

Ndugu/mlezi wa kijana yakupasa kuzingatia kuwa SHULE ITAFUNGULIWA tarehe 11/1/2021 saa moja kamili asubuhi.

Mwisho pamoja na barua hii naambatanisha kwako; kiambata MISS A,B,C,D & E.

KARIBU SANA MISUFINI SEKONDARI

.....

S.S.KITCHE

MKUU WA SHULE

NAKALA:-

AFISA ELIMU SEKONDARI (W)

S.L.P 49

NACHINGWEA

MAAGIZO YA MAHITAJI YA MWANAFUNZI

A. SARE YA SHULE

WAVULANA

- (i) Suruali mbili (2) za Darkblue zilizoshonwa kawaida zisiwe na muundo wa jinsi (Jeans) au modo pia isiwe na marinda kiunoni.
- (ii) Mashati mawili (2)ya (Tetron) Mikono mifupi.
- (iii) Viatu vya Ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi
- (iv) Soksi ndefu jozi mbili (2) nyeupe
- (v) Fulana ya shule inapatikana shuleni

WASICHANA

- (i) Sketi mbili (2) za Darkblue ndefu zinazofunika magoti rinda box
- (ii) Blauzi mbili (2) nyeupe aina ya TETRON mikono mifupi.
- (iii) Viatu vya ngozi jozi mbili (2) lakini kisigino kiwe kifupi.
- (iv) Soksi ndefu nyeupejozi mbili (2)
- (v) Fulana ya shule inapatikana shuleni

ZINGATIO

Hijabu zinaruhusiwa lakini ziwe za rangi nyeupe za tetron zilizoshonwa na nusu kanzu.

B. VIFAA VYA TAALUMA

- (i) Mkoba wa kubebea madaftari (School bag) mfuko wa plastiki hauruhusiwi.
- (ii) Madaftari makubwa kumi na moja (11) Counter books.
- (iii) Mkebe (Mathematical set)
- (iv) Kalamu za wino,za risasi, rula na vifutio
- (v) Rimu (A4) moja nyeupe

C. VIFAA VYA MICHEZO

Mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vya michezo kama vile: Bukta, full jezi,viatu vya michezo

D. VIFAA VYA USAFI NA KILIMO

Hatutampokea kijana wako kama hatafika na vifaa vya usafi na kilimo siku ya kuripoti.Vifaa hivyo ni:-

- (i) Jembe aina ya NGWAMBA na mpini wake na
- (ii) Fyekeo au Panga

Vifaa hivi vitakaguliwa pindi anaporipoti shuleni na vinakuwa vya shule baada ya kuvikabidhi.

SHERIA ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10, ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya ELIMU mafunzo ya Sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya ELIMU nchini na ofisi ya RAIS TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji ELIMU. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni na mahali popote atakiwapo.
2. Mwanafunzi avae sare ya shule wakati wote wa masomo isipokuwa wakati wa kazi za mikono na michezo tu.
3. Mwanafunzi lazima awe safi na nadhifu wakati wote.
4. Ni marufuku mwanafunzi kufuga kucha, nywele, wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele na kupaka rangi za kucha.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo na ajipangie muda wa kujisomea na kufanya mazoezi awapo shuleni na nyumbani. Mwanafunzi atakayekuwa mzembe na mvivu atachukuliwa HATUA KALI.
6. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki kikamilifu shughuli mbalimbali za shule kama vile kazi za mikono, michezo, utamaduni na za ujenzi wa TAIFA nje ya shule.
7. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtii na kuheshimu wanajumuia wote wa shule na watu wengine wote nje ya shule.
8. Kila mwanafunzi hana budi kutunza mali yake binafsi ya watu wengine na ile ya umma.
9. Ni marufuku kwa mwanafunzi kipindi cha masomo kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa, ruhusa fupi itatolewa na mwalimu wa ZAMU. Ruhusa ya muda mrefu itatolewa na MAKAMU MKUU WA SHULE baada ya maombi kupitia kwa mwalimu wa darasa na wa ZAMU.
10. HALI inaporuhusu wanafunzi wa kike watapimwa ujauzito na mganga muda wowote ili kufahamu hali zao za kimwili.
11. Ni marufuku kwa Mwanafunzi kuvuta sigara, kucheza Kamari, pool, gudugudu au kuonekana katika sehemu za starehe kama vile CLUB, GUEST HOUSE N.K
12. Mwanafunzi atafukuzwa shule mara moja akipatikana na makosa yafuatayo:-
WIZI, Uasharati na ushoga, Ubakaji, Ulawiti, Ulevi na matumiziya dawa ya kulevya, Kupigana au kupiga, Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, kudharau bendera, wimbo wa TAIFA, Fedha na picha za viongozi wa kitaifa, kupata mimba, kutoa mimba, kuo au kuolewa, kuwa na simu ya mikononi, kukataa ADHABU kwa makusudi na kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga AMANI na USalama wa shule au watu.

TAARIFA KUHUSU MWANAFUNZI

(Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi wa Mwanafunzi na iwasilishwe shuleni)

- (i) Jina la Mwanafunzi (alilotumia katika mtihani wa darasa la VII andika kwa herufi kubwa.....
- (ii) Kabila la Mwanafunzi.....
- (iii) Wilaya alikozaliwa Mwanafunzi.....Mkoa.....
- (iv) Dini ya Mwanafunzi.....
- (v) Tatizo la kiafya (eleza bayana kama lipo).....
- (vi) Jina kamili la baba Mzazi.....anuani.....
Namba ya simu.....kazi.....Umri.....
- (vii) Jina kamili la Mama Mzazi.....anuani.....
Namba ya simu.....kazi.....Umri.....
- (viii) Jina kamili au Mlezi.....uhusiano kati ya mlezi na mwanafunzi.....
- (ix) Baba na mama wanaishi pamoja/wametengana/yatima(kata isiyohusika)
- (x) Kama ni yatima ni nani:- Wote/Baba/Mama(kata isiyohusika)

AHADI YA MZAZI/MLEZI:

Mimi.....ambae ni Mzazi/Mlezi wa

Wa kijiji cha.....kata yaKatika wilaya yaNimesoma na kuyaelewa maagizo ya kujiunga na shule,hivyo nakubali/sikubali mwananguasome katika shule ya sekondari MISUFINI.Pia nipo tayari kutekeleza maagizo yote kama yalivyopangwa na shule kwa maendeleo ya shule.Nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu kumsaidia mwanangu KUTII SHERIA,TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE wakati wote atakapokuwa anasoma shuleni.

Jina la Mzazi/Mlezi(kwa herufi kubwa).....

S.L.P.....SIMU NO.....

Saini ya Mzazi/Mlezi.....Tarehe.....

Saini ya Mwanafunzi.....Tarehe.....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA NACHINGWEA

SHULE YA SEKONDARI MISUFINI,
S.L.P 73,
NACHINGWEA

KUMB.NA.MISS/BJ/VOL.2/

MZAZI/MLEZI WA.....

C/O MWL.MKUU S/M.....

S.L.P 49

NACHINGWEA.

YAH.MICHANGO YA CHAKULA

Husika na somo hapo juu.

Ninapenda kukufahamisha kuwa shule kupitia kikao cha wazazi,walimu na wajumbe wa bodi kiliamua kuwepo utaratibu wa chakula cha mchana cha wanafunzi.Hivyo kwa kuwa wewe ndio kwanza unamleta kijana wako michango ni kama ifuatavyo:-

- a) Fedha za mpishi,kusagia na manunuzi ya viungo Tsh..... Kwa mwaka.
- b) Mahindi kilo..... kwa mwaka
- c) Mboga jamii yakunde kilo..... kwa mwaka

Natanguliza shukrani,

Ahsante

.....
S.S.KITCHE

Mkuu wa Shule

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

HEADMASTER MISUFINI S.S

P.O. BOX 73

NACHINGWEA

TO DISTRICT MEDICAL OFFICER
NACHINGWEA GOVERNMENT HOSPITAL
S.L.P 30
NACHINGWEA

PART 'A'

.....(Name in full student) Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for a full secondary education

The examination should the following (i).....

- (iii) Cash category or Sub – category of which will surrender the applicant INELIGIBLE in case DEFECT. Pregnancy (category iv) will also render a girl student INELIGIBLE for the course.
- (iv) (a) Eye – Sight
- (b) Cirrhosis
- (c) Limbs
- (d) Speech
- (e) Veneral disease (VDRL)
- (f) Leprosy.....
- (g) Epilepsy.....

PART 'B'

MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by government medical offices)

I have examined the above named and consider that his/her is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNFIT for full Secondary education

- (ii) Neurosis
- (iii) Cirrhosis
- (iv) Pregnancy
- (v) Chest
- (vi) Other serious Disease

Name and Signature of medical Officer.....

Designation.....

Official stamp.....

